

**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA**  
**FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SASYAKA**

**SHULE YA SEKONDARI SASYAKA,**  
**S.L.P 599,**  
**MBEYA.**  
**TAREHE.....**

**JINA LA MWANAFUNZI.....**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA.....KATIKA**  
**SHULE YA SEKONDARI SASYAKA.**

**MZAZI/MLEZI WA.....**

Ninayo furaha kukuarifu kuwa mtajwa hapo juu amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka..... katika Shule ya Sekondari Sasyaka. Hongera na karibu sana.

Shule ipo katika Kijiji cha Masoko, Kata ya Masoko, Tarafa ya Isangati, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya. Shule itafunguliwa tarehe..... na masomo yataanza rasmi tarehe ya kufunguliwa shule.

**MAAGIZO/MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.**

**1. SARE YA SHULE.**

- a. Sare ya shule kwa wavulana ni;-
  - Suruali kijani kikavu-kitambaa original na rangi ya dhahabu (gold). Mashati rangi nyeupe mawili ya mikono mifupi.
  - Kwa wasichana watavaa sketi kijani kikavu-kitambaa original na sketi ya rangi ya dhahabu, mashati rangi nyeupe mawili ya mikono mifupi.

**NB:**

- Sketi rinda boksi, ndefu karibu na unyayo.
- Suruali ndefu isiwe ya kubana.
- Wote washone tai mbili rangi ya kijani na dhahabu.
- b. Sweta pea mbili rangi ya kijani kikavu na rangi ya maruni/damu ya mzee
- c. Viatu rangi nyeusi vya ngozi vyenye kisigino kifupi na kamba (jozi mbili).
- d. Soksi nyeupe (jozi mbili)
- e. Wavulana watavaa mkanda mweusi wa ngozi
- f. Sare ya michezo Truck suit rangi ya kijivu kwa wavulana, na wasichana (isiwe ya kubana). Raba jozi moja, bukta kwa wavulana.
- g. Aje na kamusi (Dictionary) moja, mkebe(mathematical set) moja, four figure (mathematical table) moja, pia aje na daftari kubwa (counter book) kumi, faili dogo moja kwa ajili ya kutunzia matokeo ya mitihani yake.
- h. Aje na passport size (picha ndogo) nne.
- i. Aje na begi la kubebea daftari zake.

**KUMBUKA:** Hakikisha ana mahitaji yote, na vifaa vyote vitakaguliwa pindi utakapo mleta mwanao shuleni siku ya kwanza.

Imetolewa na,

.....  
**MKUU WA SHULE SASYAKA SEKONDARI**  
**0743 277 192**